JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS –TAMISEMI

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

SHULE YA SEKONDARI DUMBETA

S.L.P 13,

KATESH –HANANG

25/11/2021

KUMB.Na.DSS/FOS/Vol/10

MWANAFUNZI……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2022.

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Dumbeta. Shule itafunguliwa tarehe 17/01/2022.

Mwanafunzi atakaye chelewa baada ya tarehe hiyo hata pokelewa.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A. MAAGIZO YA KAMATI YA CHAKULA.
CHAKULA.

i.Mahindi debe nne (4) kwa mwaka- mbili kwa muhula.

ii.Maharagwe debe mbili (2) kwa mwaka- moja kwa muhula.

Fedha za chakula ni Tsh. 30000/= kwa muhula na Tsh. 60000/= kwa mwaka. Fedha zote zipelekwe BANK YA NMB tawi la Katesh. Jina la akaunti ; CHAKULA DUMBETA SEKONDARI; Akanti No. 41010006289. Mwanao aje na pay slip ya benki. Pay slip itapokelewa na mhasibu wa kamati ya chakula.

B. SARE ZA SHULE.

Sare ya shule hii ni:

i. Sketi ya daki bluu mshono wa rinda boks yenye urefu jicho la mguu(ankle) kwa wasichana na blauzi ya rangi nyeupe yenye mikono mifupi.
ii. Kwa wavulana ni suruali ya daki bluu yenye selebration na isiyo simple jeans wala mnyonyo. Shati nyeupe yenye mikono mifupi na tai ya rangi ya suruali kwa wavulana na tai ya rangi ya sketi kwa wasichana.
NB. Mwanafunzi atakaye vaa sare tofauti na zilizotajwa hatapokelewa.
iii. Sweta ziwe na rangi ya daki bluu.

C. **SARE ZA MICHEZO**.

A.WASICHANA

-Sketi moja rangi ya kijani
-Fulana moja ya rangi ya kijani
-Raba ya michezo rangi yoyote

B.WAVULANA

-Bukta moja rangi ya kijani
-Fulana moja rangi ya kijani
-Raba ya michezo rangi yoyote

C. VIFAA VYA DARASANI

-Daftari kubwa 15
-Mathematical set
Kamusi ya kiingereza

D.MAENDELEO YA TAALUMA

Mwanafunzi wa shule ya sekondari dumbeta anapaswa kujibidiisha katika masomo yake wakati wotena kufaulu vizuri mitihani ya kila mwezina mwisho wa muhula/mwaka. Mwanafunzi anapaswa kupata wastani wa 50% hadi 100% katika maendeleo yake kitaaluma.

Mwanafunzi atakaye shindwa kufikia wastani wa alama hizo yaani wastani wa 50% atapaswa kuja na mzazi wake shuleni ili kushauriana na uongozi. Taarifa kuhusu maendeleo yako kimasomo , tabia na kazi za mikono itatumwa kwa mzazi /mlezi wako aliyeandikiswa shuleni naye atatakiwa kuwa ameipokea na atoe maoni yake kuhusu hilo bila majibu hatapokelewa shuleni.

Mwanafunzi haruhusiwi kutoka shuleni bila ruhusa.

VIAMBATANISHO MUHIMU.

1.Cheti cha dakitari fomu namba moja imeambatanishwa.
2.Fomu na 2.ya mapokezi shuleni imeambatanishwa.

FOMU ZOTE ZIJAZWE KIKAMILIFU

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI DUMBETA.

…….

M/ MKUU WA SHULE

SHERIA NA KANUNI ZA ZA SHULE

1.Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu No.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a)Heshima kwa viongozi wa nchi , waalimu, wazazi ,wafanyakazi wote ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b.) Mahudhurio mazuri kwa kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

(c) Kuheshimu NEMBO, NYIMBO, BENDERA, PICHA ZA VIONGOZI WA TAIFA NA FEDHA ZA TAIFA.

(d). Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha ya matusi kwa mwalimu, watumishi wasio walimu, wageni na wanafunzi wenzake.

(e) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazo pewa.

(f). Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(g). Kutunza usafi wa mwili na mzingira ya shule.

(h). Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.

(i). Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(j). Kunyoosha mkono pindi anapouliza swali au kujibu swali.

(k). Kutoa taarifa ya afya yake bila kuficha kitu chochote.

(l). Kuheshimu mahali pa kulia chakula(bwalo), vyumba vya madarasa, ofisi na mali za umma na binafsi.

(m) Kuheshimu na kutekeleza sheria nyingine zozote ndogondogo utakazo zikuta shuleni na viongozi wa SERIKALI YA WANAFUNZI.

2. MAKOSA YANAYOWEZA KUKUSABABISHIA KUFUKUZWA SHULE

-Wizi

-uasherati na ushoga

-ubakaji ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k

-kupigana au kupiga

-Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

-Kudharau bendera ya taifa

-Kuoa au kuolewa

-Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.

-Kutoa mimba.

-Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

-Kukataa adhabu kwa makusudi.

- kumiliki simu ya mkononi.

FOMU NA 1

1.IJAZWE NA MGANGA MKUU / WILAYA /KITUO CHA AFYA.

MWANAFUNZI AJE NAYO NA KUMPA MKUU WA SHULE.

(USIPIMWE KWINGINE KOKOTE)

Mimi ni (jina la mganga mkuu wa mkoa/ kituo cha afya……

Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi…….

Amepimwa kikamilifu na kuonekana kuwa anayo/ hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo:

HALI YA MWILI

1.Mapigo ya moyo……..

2.kiasi cha damu……

3. kundi la damu……

4.mkojo …….

5.Kinyesi……

6. Macho……

7.masikio……..

ANGALIZO: Weka maoni yako katika kila kipengele tajwa.

b. MAGONJWA

Amewahi/anayo/hana magonjwa yafuatayo.

a. Pumu……
b. kifua kikuu……
c. Kifafa……
d. Shinikizo la damu chini/ juu……
e. Vidonda vya tumbo……
f. Sickle cell……..
g. Ukoma……
h. Magonjwa ya zinaa……
i. Magonjwa ya kili……
j. M aradhi mengine makali yasiyo tajwa hapo juu……

Sahihi na muhuri wa daktari/ mganga

Tarehe……

FOMU NA 2

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKLI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

SHULE YA SEKONDARI DUMBETA

S.L.P 13

KATESH- HANANG

TAREHE…….

Kumb. Na.DSS/F/SEL./VOL. 1……

FOMU YA MAPOKEZI SHULENI –MAELEKEZO KUHUSU MWANAFUNZI

SEHEMU A: IJAZWE NA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI (andika majina matatu kwa herufi kubwa)……..
2. Uraia……..
3. Tarehe ya kuzaliwa……
4. Shule anayotoka……..
5. Tarehe ya kutoka shule hiyo……..

SEHEMU B. IJAZWE NA MZAZI / MLEZI

1.Jina lamzazi/ mlezi……..
2. Anwani ya mazazi /mlezi…….
3.Kazi ya mzazi /mlezi……..
4.Mahali anapofanyia kazi……..
5. Mahali anapoishi (kijiji au kata)…….
6.Ndugu wawili wa karibu (wanaoweza kufanya majukumu ya mzazi/ mlezi kuhusu mwanafunzi

1. Ndugu wa kwanza;
   Jina……
   Anwani……..
   Uhusiano wake na mwanafunzi…….

Uhusiano wake na mzazi…….

2.Ndugu wa pili

Jina……

Anwani……

Uhusiano…….

Uhusiano wake na mwanafunzi……

Uhusiano na mzazi……